4. Kwamba Kristo aliishughulikia *dhambi ya asili* kwa utoshelevu na kutwaa adhabu ya dhambi milele, ili mwanadamu ashinde kikamilifu dhambi zote halisi zitakazotendwa baada ya ubatizo pamoja na kuzibeba adhabu za kitambo kidogo: Kanisa la Katoliki la Roma. Ebrania 10:10-14; 1 Pet. 3:18; 1 Yn. 2:1-2; Rum. 5:10.

5. Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya wateule tu na kusamehe kikamilifu dhambi zao tu: Makanisa ya Kikalvini, Wapresbiteriani, Congregational Christians, Wabatisti wa asili ya Kalvini, Wamethodisti wa asili ya Kalvin, Waaldensia. 2 Kor. 5:15-18; Yn. 1:29; 1 Tim. 2:5-6; Rum. 8:32; Ebr. 2:9; Tito. 2:11; 2 Pet. 2:1.

6. Kwamba kifo cha Kristo pekee hakitoshi kusamehe dhambi zetu, bali msamaha ni neema ya Baba tu: Waarmenia. Rum. 5:10, Yn. 19:30; 1 Pet. 2:24.

7. Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, lakini kikomo cha upatanisho ni kwa waaminio tu na kwamba

upatanisho huo ulianza mwaka wa 1844. Wasabato. Ebr. 1:3; Rum. 8:34; 1 Tim. 4:10; Tito. 2:11; 2 Pet. 2:1; 1 Kor. 15:57; 1 Yn. 1:7.

8. Kwamba Kristo hakutosheleza msamaha kwa ajili ya dhambi za mwanadamu, kwa hiyo utoshelevu huo hauhitajiki. Wayunitariani, Wayunivestalisti, Waprotestanti Huru, Shakers, Spiritists, Wamodenisti. Zab. 49:8-9; Uf. 14:13:(5:9); Isa. 53:6; Rum. 3:23-26; Mdo. 4:12; Mat. 20:28; 1 Tim. 2:6; Rum. 8:32, 2 Kor. 5:19-21.

9. Kwamba kwa kufa kwake Kristo hakulipia adhabu ya dhambi zetu, bali aliuwezesha upendo wa Mungu kumsamehe mwenye dhambi atubuye. Jeshi la Wokovu na Wakalvinisti wengi. 2 Kor. 5:14-15; Yn. 1:29; 1 Yn. 3:8.

10. Kwamba Kristo hakutukomboa kwa mateso na kufa kwake, bali ametuwekea nafasi tu katika Utawala wake (Millenium) ili turithi uzima wa milele kwa njia ya utii wetu wenyewe. Waruselaiti (Rusellites), Isa. 53:6; Mat. 20:28; Yn. 14:6; Lk. 16:26; 1 Yn. 1:7; 1 Yn. 2:1-2.

11. Kwamba Kristo si Mpatanishi pekee kati yetu na Mungu, kwa hiyo watakatifu pia ni wapatanishi, na hasa Maria, ambaye ustahili wake ni wa thamani kubwa mbele ya Mungu kiasi cha kuweza kutuombea: Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki. Yn. 14:6; Mdo. 4:12; 1 Tim. 2:5.

12. Kwamba Kristo si Mwokozi pekee wa ulimwengu: Wamodenisti, Shakers. Isa. 42:8; Isa. 43:11.

13. Kwamba ubinadamu wa Kristo ulipewa sifa/tabia ya kiungu zilizokoma wakati wa kutukuzwa kwake: Makanisa ya Kikalvini, Schwenkfeldians. Zab. 102:27; Ebr. 1:12-13; Efe. 1:20-21.

14. Kwamba katika hali yake ya ubinadamu wakati wa kuteswa (kudhalilishwa) kwake, Kristo hakuwa na ukuu wa kimungu, kwa sababu uwezo huo alipewa wakati wa kutukuzwa kwake tu: Waarmenia, Evangelical Congregational, Campbelittes, Irvinginites, Makanisa ya Kikalvinisti kwa ujumla. Yn. 2:11; Yn. 18:6; (Isa. 9:6-7).

15. Kwamba nafsi ya Kristo haikuonja maumivu wakati wa mateso: Kanisa la Roma Katoliki. Mat. 27:46; Mat. 26:38; Lk. 22:42; Ebr. 2:17-18; (Ebr. 5:7-8).

16. Kwamba ghadhabu ya Mungu haikuwa juu ya Kristo wala mateso ya jehanamu (motoni) hayakumpata: Wayunitariani, Waarmenia, Ushirikiano wa Kiinjili, Wayunivestalisti, Waprotestanti Huru, Wamodenisti. Gal. 3:13; Gal. 3:10; Rum. 6:23; (Zab. 16:10).

17. Kwamba baada ya kifo nafsi ya Kristo iliingia kuzimuni (*limbus patrum*) ili kuwafungua na kuwaweka huru watakatifu wa Agano la Kale. Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Katoliki la Mashariki. 1 Pet. 3:18-19; Kol. 2:15; 1 Kor. 15:55; (Lk. 16:23).

18. Kwamba kwa hakika Kristo hakushuka kuzimu: Makanisa ya Kikalvinisti, Waarmenian, Wayunitarian, Evangelical Congregational Church. Efe. 4:9; 1 Pet. 3:18-19; Kol. 2;14.

19. Kwamba Kristo hakufufuka kimwili toka kwa wafu: Waruselaiti, Christian Scientists. Yn. 2:19; Waf. 3:20-21; Mat. 28:2ff; Yn. 20:19-26; Mat. 17:1ff; (Zab. 16:9-11).

20. Kwamba baada ya kutukuzwa Kristo alikuwa na mwili mpya tofauti na mwili aliokuwa nao awali: Wayunitarian. Lk. 24:39; Waf. 3:8-9; Mdo. 7:55.

21. Kwamba kuketi kwa Kristo katika mkono wa kuume (wa Mungu) hakumaanishi mamlaka aliyonayo juu ya ulimwengu, wala nguvu na ukuu na enzi, (kulingana na hali ya ubinadamu), bali ni uwezo wenye ukomo na mipaka ya sehemu iliyo yake mbinguni: Makanisa ya Kikalvinisti, Waanglikana, Congregational Christians, Wababtisti, Wamethodisti, Evangelical Congregational, Waarmenia, Unitarians (wasioamini Utatu Mtakatifu), Wasabato, n.k. Zab. 110:1; Ebr. 1:3; Efe. 1:20-23; 1 Pet. 3:22.

22. Kwamba Kristo hayupo ulimwenguni, bali anawakilishwa na Roho Mtakatifu: Wamomeni. Mat. 28:20.

## IX YAHUSUYO KUZALIWA MARA YA PILI/ KUBADILIKA KIIMANI

**TUNAAMINI KWAMBA** (a) imani iokoayo ndani ya Kristo haipatikani kwa ama ndani ya mwanadamu yeyote, bali ni karama ya Roho Mtakatifu inayotolewa bure wakati wa kuzaliwa mara ya pili; (b) kuzaliwa mara ya pili si kazi ya mwanadamu, bali ni kazi ya Mungu, ambaye kwa neema na kwa nguvu yake, kwa njia ya Kristo, huwabadilisha wenye dhambi kwa Injili; (c) Roho Mtakatifu hufanya kazi ya kubadilisha si watu wachache tu, bali wasikiaji wote wa Neno, na iwapo baadhi ya wasikiaji hawaokolewi ama kubadilika hiyo haitokani na upungufu wa neema ya Mungu bali ni matokeo ya ukaidi na upinzani wao. (d) Tunakataa mafundisho yote yenye twaswira mbili tofauti kwamba kubadilishwa (okolewa) hakuletwi moja kwa moja na neema ya Mungu, ila kwa kiasi fulani kunachangiwa na juhudi ya mwanadamu kwa tabia njema, uamuzi binafsi na kutokuwa na hatia kwa kulinganishwa na wengine. (e) Tunakataa pia mafundisho ya Kikalvini yanayosema kwamba kwa hakika Mungu hatawaokoa wasikiaji wote wa Neno, isipokuwa wateule tu.

a) 1 Pet. 1:3-4 Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.

Yn. 3:5-6 Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni Roho.

Efe. 2:1 Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; (Tazama pia Yak. 1:18; Zab. 103; Yn. 8:21; Zab. 51:7; Zab. 51:12; Yer. 31:18; Rum. 3:23; Rum. 7:18.

b) 1 Kor. 2:14 Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.

Efe. 1:19-20 Na ubora wa uwezo wa ukuu wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho.

Rum. 10:17 Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.

c) Mat. 23:37 Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!

Mdo. 7:51 Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo.

d) 1 Kor. 2:14 Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.

Efe. 4:18 ambao akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao.

Waf. 2:13 Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema (Tazama pia Lk. 19:41-42; Rum. 3:23; Rum. 8:7).

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba kuzaliwa mara ya pili si kazi ya Mungu pekee, bali kwa sehemu ni kazi ya mwanadamu. Wakempbelaiti, Wapresbiteriani, Watetemekaji, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Shakers, Unitarians, Synergists, Waroma na Makanisa ya Orthodox ya Mashariki, Waarmenia, Modernists, Wamenonaiti, Free Will Baptists, Wamomeni, Wasabato, Ushirika wa Kiinjili, Universalists, (See passages above).

2. Kwamba watoto hawawezi kuokolewa: Unitarians, Wakempbelaiti, Wabatisti. Mk. 10:14; Mat. 18:10-11; (Tazama pia Isa. 28:9).

3. Kwamba haiwezekani mtu akapoteza imani akiishaokolewa na kwamba mtu akianguka hawezi kuipoteza neema. Makanisa ya Kikalvini, Wakempbelaiti, Wapresbetariani n.k. Gal. 4:19, Lk. 8:13. (Tazama pia Mwanzo 3).

4. Kwamba wito kwa wasio wateule si wa kweli wala wa dhati kwa hiyo hauwezi kuwa na matokeo yanayotarajiwa: Makanisa ya Kikalvini, Wapresbeteriani, Congregational Christians, Wabatisti wa Kikalvini. Mat. 11:28; Mk. 16:15-16; Mdo. 17:30; Mat. 28:19-20. (Mithali 1:24; Isa. 1:5; 18-20; Ezek. 33:11).

5. Kwamba Roho Mtakatifu huumba imani na toba lakini si kwa njia ya Neno la Mungu, bali kwa mwanga wa ndani ambao Roho Mtakatifu huwapa mwanadamu: Watetemekaji (Quakers). Rum. 10:17; Yak. 1:18; 1 Pet. 2:2.

6. Kwamba imani si karama itokanayo na neema ya Mungu Roho Mtakatifu pekee, bali mwanadamu anaweza kuiamini Injili pasipo Roho Mtakatifu: Unitarians, Wakempbelaiti, Waarmenia, Wapresbeteriani wa Cumberland. 1 Kor. 12:3; Kol. 2:12; Mat. 16:17; Yn. 6:44, 65.

7. Kwamba neema ya Mungu iokoayo haizuiliki ama kupingika: Makanisa ya Kikalvini, Congregational Christians, Wabatisti wa Kikalvini, n.k. Isa. 65:2; Lk. 7:30; Yn. 5:40; (Mdo. 7:51).

## XII. YAHUSUYO IMANI NDANI YA KRISTO

**TUNAAMINI** (a) kuwa kwa njia ya Kristo mwanadamu amepatanishwa na Mungu na upatanisho huo unatangazwa kwa wanadamu kwa njia ya Injili na kwa utimilifu wake wanadamu wote wanapaswa kuuamini ujumbe wa neema ya Mungu, *na kwamba imani ndani ya Kristo ni njia pekee ya kupata msamaha wa dhambi na wokovu;* (b) kwamba imani ndani ya Kristo ni kuamini pasipo shaka msamaha wa dhambi kwa njia ya Kristo peke yake.

a & b) Mdo. 10:43; Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi.

Yn. 3:16-17, 36 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele.

Ebr. 11:1 Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. (Tazama pia Rum. 4:20-21).

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba imani haitokani na kuamini Injili bali kukubali mafundisho kama yanavyofundishwa na Kanisa: Kanisa la Roman Katoliki. Yn. 3:36; Rum. 4:20-21; 2 Tim. 1:12; Yn. 20:28ff.

2. Kwamba imani iokoayo haitokani na mwenye dhambi kuamini kuwa msamaha wa dhambi zake unatokana na Kristo, bali kuikubali Injili: Kanisa la Roman Katoliki, Universalists, n.k. Rum. 8:38-39; Ebr. 10:22; (Rum. 5:4; Ebr. 6:18; 10:38-39).

3. Kwamba kiini cha imani si Kristo msulibiwa na haki yake: Unitarians, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Watetemekaji (Quakers), Modernists. Mdo. 16:31; Rum. 3:24-25; Gal. 2:20; (1 Kor. 1:18-23; 2:2).

4. Kwamba upendo na utii ni asili ama kiini, na si matunda ya imani: Unitarians, Waarmenia, Kanisa Roman Katoliki, Wamenonaiti, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Modernists. Gal. 5:4-6; Ebr. 11:1.

5. Kwamba imani iokoayo pamoja na dhambi ya kufisha kwa pamoja zinaweza kuwemo ndani ya mioyo ya wateule: Kanisa Katoliki la Roma, Makanisa ya Kikalvini, Yn. 2:3-4; 1 Yn. 3:36, (Rum. 3:31; Yak. 2:14-26; Efe. 2:10).

## XIII YAHUSUYO KUHESABIWA HAKI

**TUNAAMINI** (a) kwamba Mungu hawapokei wanadamu kwa msingi wa matendo yao mema, (b) bali pasipo matendo ya Sheria, kwa neema tu, na kwa ustahili mkamilifu unaotokana na Kristo. Kristo huwahesabia haki kwa kuwatambua wote wanaoamini kuwa wenye haki na kwamba kwa ajili yake Kristo dhambi zao zimesamehewa. (c) kwamba kwa fundisho hili Kristo anapewa heshima anayostahili, na kwa njia yake tu wenye dhambi hupokea faraja idumuyo yaani uhakika kwamba Mungu ni mwenye neema kwao.

a) Zab. 130:3-4. Bwana, kama wewe *ungehesabu maovu*, Ee Bwana, *nani angesimama?* Lakini kwako kuna msamaha, ili wewe uogopwe.

Zab. 31:1. *Nimekukimbilia wewe, Bwana,* nisiaibike milele. Kwa haki yako uniponye.

Zab. 143:2. Wala *usimhukumu* mtumishi wako, maana kwako hakuna aliye hai mwenye haki.

b) Rum. 3:28. Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria.

Rum. 3:22-24. Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. *Maana hakuna tofauti; kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake*, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.

1 Kor. 1:30. Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi. Rum. 8:33-34.

c) 1 Tim. 2:5 Kwa sababu *Mungu ni mmoja*, na *mpatanishi* kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.

Rum. 8:38-39 Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala *uzima*, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza *kututenga na upendo wa Mungu* ulio *katika Kristo Yesu Bwana wetu.*

2 Kor. 1:19-20 Maana Mwana wa Mungu kristo Yesu aliyehubiriwa katikati yenu na sisi, yaani, mimi na Silwano na Timotheo, hakuwa ndiyo na siyo; bali katika yeye ndiyo. Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi. (Tazama pia Rum. 3:22-25).

d) Rum. 3:28. Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria.

2 Tim. 1:9. Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi tuliyopewa katika Kristo Yesu tangu milele.

Rum. 4:5. Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali amwaminiye yeye ambaye amehesabiwa haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki.

Efe. 2:8-9. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu.

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba kuhesabiwa haki si tendo la Mungu mwenyewe ambalo kwa njia yake huwapa waaminio haki ya Kristo, bali linategemea kugeuzwa na kutakaswa kwa njia ya neema inayoshindiliwa (tiwa) moyoni mwa mwenye dhambi. Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki, Wamenonaiti, Irvingites, Watetemekaji (Quakers), makanisa ya Yerusalemu Mpya, Schwenkfeldians, Jeshi la Wokovu. Rum. 8:33-34; (Rum. 11:6).

2. Kwamba kwa hakika dhambi zimesamehewa lakini si kwa ajili ya Kristo wala si kwa kuhesabiwa haki kwa ajili yake: Unitarians, Waarmenia, Modernists, Universalists. Efe. 1:7; Rum. 11:6; Mdo. 10:43; 2 Kor. 5:21; Waf. 3:9.

3. Kwamba kuhesabiwa haki hakujumuishi msamaha wa wakati huu wa sasa (kwa sababu ondoleo la dhambi halikamilika bado), bali ni katika ahadi ya msamaha kwa wakati ujao ambao wameahidiwa wale wanaotubu na kuziacha dhambi: Wasabato, Rum. 3:24,35; (Zab. 103:3).

4. Kwamba dhambi hazijasamehewa badala yake zimeangamizwa: Christian Scientists. 1 Yn. 1:8-9.

5. Kwamba katika kusamehe dhambi Mungu hafuti adhabu zote, bali mwanadamu mwenyewe anapaswa kulipia kwa ukamilifu msamaha wa adhabu za muda wa sasa: Kanisa la Roman Katoliki, Universalists. Efe. 2:4-5; 1 Yn. 4:10; Kol. 2:13; Rum. 4:5; Rum. 10:4; (Ebr. 10:14).

6. Kwamba mwanadamu anahesabiwa haki, lakini si kwa sababu ya imani inayotegemea ustahili wa Yesu, bali ni kwa ajili ya utii wa hiari kwa Neno lake: Kanisa Katoliki la Mashariki, Wamenonaiti, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Wasabato, Wamomeni, Irvingites, Waarmenia, Unitarians,

Waprotestanti Huru, Wakempbelaiti. Waf. 3:9; Mdo. 10:43; Efe. 2:8-9; Rum. 4:16; (Rum. 10:14).

7. Kwamba mtu anahesabiwa haki kwa njia ya "matendo ya imani," na kwamba wokovu wa mtu unategemea matendo mema: Wakempbelaiti, Watetemekaji (Quakers), Wakristo wa Kiisraeli: Rum. 3:22; (Rum. 11:6).

8. Kwamba Mkristo hawezi kuwa na uhakika wa msamaha wa dhambi zake, na kwa ajili hiyo analazimika kuwa na mashaka kuhusu wokovu wake: Kanisa la Roman Katoliki. Rum. 5:1-2; Rum. 8:15-16.

9. Kwamba mwenye hakika na msamaha wa dhambi ni yule anayehisi neema ya Mungu moyoni mwake: Wamethodisti; Wamoraviani, Evangelical Congregational, Jeshi la Wokovu, Makanisa ya Kikalvini: Yn. 20:29; 1 Yn. 3:20; Rum. 4:18-22; Yak. 1:6; (Zab. 51:3-8, 10-12; Zab. 28:1).

## XIV YAHUSUYO TOBA

**TUNAAMINI** (a) kwamba toba ni kumgeukia Mungu kwa njia ya imani katika Kristo pale ambapo kwa njia ya sheria mwenye dhambi anatambua dhambi zake na kuzijutia: (b) kwamba toba inaambatana na mambo mawili yaani majuto na imani; (c) kwamba kujuta ni huzuni ya kweli na ya uaminifu, inayotokana na dhambi kuwekwa bayana kwa njia ya sheria ya Mungu, kuogofwa na ghadhabu na adhabu ya Mungu iliyo ya haki: kwamba imani ni tendo la nafsi ambayo neema na rehema ya Mungu vinakaa ndani yake kwa nguvu ya Roho Mtakatifu kama ilivyo katika Injili kwa kusudi la kuupata uzima wa milele.

a) Luka 18:13. Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, *wala hakuthubutu*
*hata kuinua macho yake mbinguni*, bali alijipiga-piga kifua kifua akisema, Ee Mungu, *uniwie radhi mimi mwenye dhambi.*

b & c) Zab. 51:17. Dhabihu za Mungu *ni roho iliyovunjika*; *moyo uliovunjika na kupondeka*, Ee Mungu, hutaudharau.

Mdo. 16:30-31. Kisha akawaleta nje akasema, Bwana zangu yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, *mwamini Bwana Yesu*, nawe *utaokoka* pamoja na nyumba yako.

d) 2 Tim. 1:12. Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana *namjua yeye niliyemwamini*, na *kusadiki ya kwamba aweza kukilinda nilichokiweka* amana kwake hata siku ile.

1 Kor. 12:3. Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema, Yesu amelaaniwa; *wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu.*

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba toba ni Sakramenti ya Agano Jipya kwa ajili ya dhambi za mauti zilizotendwa baada ya ubatizo, na kwamba inajumuisha majuto ya moyo, kuungama dhambi zote mbele ya Paroko (Padre) na kufanya matendo mema: Kanisa la Romani Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki. Mdo. 19:4; Uf. 2:5; Isa. 54:10; (66:2; Hos. 14:2); Luka 24:46-47; Heb. 11:6; (Yer. 31:19).

2. Kwamba imani si muhimu kwa toba (yaani toba haihusiani na imani): Makanisa ya Kikalvini, Wamethodisti, Evangelical Congregational Church, Wamoraviani, Jeshi la Wokovu, Free Will Baptists. Mat. 3:2; Mat. 5:6, Yn. 3:16.

3. Kwamba kimsingi toba ni pamoja na kuacha dhambi na kufanywa upya moyoni. Kanisa la Roman Katoliki, Kanila la Orthodox la mashariki, Wamenonaiti, Wamomeni, Free Will Baptists, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Unitarians, Universalists, Waprotestanti Huru, Wasabato, Wakempbelaiti, Calvinistic Reformed Churches, Wamethodisti, Evangelical Congregational, Wamoraviani. Zab. 6:3-4; Rum. 4:6; (1 Wafalme 8:47; Eze. 14:6; Lk. 17:4; Mdo. 26:20).

## XV. YAHUSUYO UTAKASO NA MATENDO MEMA

**TUNAAMINI** (a) kwamba matendo mema ni matokeo ya kuokolewa kwa imani ya kweli ambayo hutokana na nguvu ya Roho Mtakatifu kulingana na amri za Mungu kwa kusudi la kumtukuza Mungu na kuonyesha shukrani (b) kwamba kwa kuwa utakaso katika maisha haya si mtimilifu (unaweza kutiwa dosari), vivyo hivyo matendo ayafanyayo mtu aliyeongolewa huweza kutiwa dosari kwa udhaifu wa mwili; (c) kwamba matendo mema sharti yatendwe, si kwa kusudi la kupokea

msamaha wa dhambi au kununua uzima wa milele, bali yaonyeshe imani na shukrani kwa ajili ya mema ya Mungu yaliyopokelewa na yule aliyeokolewa.

a) Mat. 15:9. Nao *waniabudu bure*, wakifundisha *mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*

Yn. 15:5. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, *akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana*; *maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.*

1 Kor. 10:31. Basi, mlapo au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. (Tazama pia Kol. 3:7).

b) Rum. 7:21-24. Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, *lipo lililo baya*. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani, *lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu*, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, maskini mimi! Ni nani *atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?*

Gal. 5:17. Kwa sababu *mwili hutamani ukishindana na Roho*, na Roho kushindana na mwili; *kwa maana hizi zimepingana*, hata *hamwezi kufanya* mnayotaka.

c) Mat. 5:16. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate *kuyaona matendo yenu mema*, *wamtukuze Baba* yenu aliye mbinguni.

Efe. 2:8-9. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala *si kwa matendo*, mtu awaye yote asije akajisifu.

Efe. 2:10. Maana tu *kazi yake*, *tuliumbwa katika Kristo Yesu*, *tutende matendo mema*, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.

Yak. 2:17-18. Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake. Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami *nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.*

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba utakaso mkamilifu na matendo mema yanawezekana katika maisha haya: Kanisa la Roman Katoliki, Waarmenia, Wamethodisti, Evangelical United Brethren, Evangelical Congregational, Jeshi la Wokovu, Schwenkfeldians, Unitarians, Wamomeni, Shakers, Holiness Churches. Waf. 3:12; 1 Thes. 4:1; 2 Kor. 4:16; Efe. 4:15; Yak. 3:2; (Yer. 17:9; Rum. 8:7).

2. Kwamba hata wasiozaliwa mara ya pili (okolewa) wanaweza kutenda matendo mema: Waarmenia, Wakempbelaiti, Unitarians, Makanisa ya Yerusalemu Mpya, Quakers. Efe. 2:10; Rum. 14:23; Mat. 7:16; Yn. 15:5.

3. Kwamba matendo yoyote mema yanahesabiwa kuwa ni matendo mema hata kama yametendwa pasipo amri maalum ya Mungu ili mradi yanalingana na maagizo ya Kanisa: Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki. Kol. 2:16-23; 1 Tim. 4:1-5.

4. Kwamba mtu mwadilifu aweza kufanya matendo ya ziada kwa ajili ya faida ya wengine: Kanisa la Roman Katoliki. Isa. 64:6; Luka 17:10; Zab. 49:7-8.

5. Kwamba matendo mema ya Mkristo ni safi na matakatifu: Quakers, Ebr. 12:1; Rum. 7:8-23; Gal. 5:17; (Isa. 64:6).

6. Kwamba matendo mema ni sharti la kupata wokovu: Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki, Waldensians, Wamenonaiti, Wakempbelaiti, Wasabato, Quakers, Makanisa ya Yerusalemu, Wamomeni, Christian Israelites. Mat. 5:16; Efe. 2:9-10; Yn. 3:16; Habakuki 2:4; Yn. 3:36. Pia Lodgery, Modernists, and Sectarian Churches kwa ujumla.

## XVI YAHUSUYO SALA/MAOMBI

**TUNAAMINI** (a) kwamba sala ni ibada takatifu ambayo kwayo Wakristo humwita Mungu wa kweli na aliye hai kwa ujasiri kwa jina la Mpatanishi Yesu Kristo kwa ajili ya mahitaji yao, na pia kwa njia hiyo kumsifu na kumshukuru kwa baraka wanazopokea maishani mwao: (b) kwamba Wakristo wanapaswa kujiombea na kuwaombea wengine bila ubaguzi,

na hasa wale walio wa nyumba ya imani; (c) kwamba Wakristo wasiwaombee wafu: (d) kwamba Wakristo wanapaswa kuomba kila wakati na kila mahali kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya wengine, na kumtegemea Kristo na kumwachia Mungu namna na wakati atakapowapa mahitaji yao.

a) Zab. 10:17. Bwana, *umeisikia tamaa ya wanyonge*, utaitengeneza mioyo yao, utalitega sikio lako.

Zab. 27:8. Uliposema, *nitafuteni uso wangu*, *moyo wangu umekuambia*, *Bwana, uso wako nitautafuta*.

Waf. 4:6. Msijisumbue kwa neno lolote; *bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru*, *haja zenu na zijulikane* na Mungu.

b) 1 Tim. 2:1-3. Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike *kwa ajili ya watu wote*; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu.

c) Ebr. 9:27. Na kama vile watu wanavyowekewa kufa *mara moja*, na baada ya kufa *hukumu*.

d) 1 Tim. 2:8. Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano.

## XVII YAHUSUYO VYOMBO VYA NEEMA

**TUNAAMINI** (a) kwamba Mungu hatoi baraka za kiroho zinazodhaminiwa na Kristo, kama vile msamaha wa dhambi, Roho Mtakatifu n.k., isipokuwa vyombo vya neema vilivyowekwa wakfu na yeye; (b) kwamba vyombo hivi vya neema ni Injili, na Sakramenti za Ubatizo na Chakula cha Bwana; (c) kwamba Injili kuwa chombo cha neema kunathibitishwa kikamilifu na Mdo. 20:24-32; Rum. 10:17; na kuhusu Ubatizo kuwa chombo cha neema inathibitishwa katika Mdo. 2:38; Tito. 3:5; na kuhusu Chakula cha Bwana inathibitishwa katika Luka 22:19-20; Mat. 26:28; (d) kwamba kwa sababu hii, yaani kwa kusema Injili na Sakramenti hizi ni

vyombo pekee vya neema vilivyowekwa wakfu na Mungu, Kristo analiagiza Kanisa kwenda ulimwenguni pote kuihubiri Injili na kutoa Sakramenti hizo (Marko 16:15-16; (e) kwa hiyo basi, vyombo vingine vyote vilivyowekwa na wanadamu ili kulijenga Kanisa ni "vipimo vipya" ambavyo kwavyo Kanisa halijengwi, bali linabomolewa.

a) 1 Kor. 1:21. Kwa maana *katika hekima ya Mungu*, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa *waaminio kwa upuuzi* wa lile neno *linalohubiriwa*.

1 Kor. 12:13. Kwa maana katika Roho mmoja *sisi sote tulibatizwa* kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; *nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja*.

b & c) Mdo. 20:24, 32. Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza *mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu*. Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa *neno la neema yake*, ambalo *laweza kuwajenga* na *kuwapa urithi* pamoja nao wote waliotakaswa.

Rum. 10:17. Basi imani, chanzo chake ni *kusikia*; na kusikia huja kwa *neno la Kristo.*

Mdo. 2:38. Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Mat. 26:28. Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya weingi kwa ondoleo la dhambi (Tazama pia Tit. 3:5; Luka 22:19-20).
d) Marko 16:15-16. Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, *mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe*. Aaminiye na *kubatizwa ataokoka*; asiyeamini, *atahukumiwa*.

e) 1 Kor. 3:11 Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo. (Yn. 6:63b. Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima).

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba zipo Sakramenti saba na kwamba hizo ndizo vyombo vya neema: Waroma na Makanisa ya Orthodox ya Mashariki. Mat. 28:19; Mat. 26:26-28.

2. Kwamba Sakramenti, yaani Ubatizo na Chakula cha Bwana si vyombo vya neema ambavyo kwa njia yake Mungu huwapa waaminio neema na Roho wake. Makanisa ya Kikalvini, Wapresbeteriani, Congregational Christians, Wabatisti, Wamenonaiti, Wamethodisti, Evangelical United Brethren, Evangelical Congregational Church n.k. (Tazama vifungu vya juu).

3. Kwamba Mungu hatoi baraka za kiroho zilizonunuliwa na Kristo mwenyewe kwa njia ya vyombo hivyo vya neema, bali pia hutoa mara moja kwa njia ya vyombo hivyo vya neema. Makanisa ya Kikalvini, Wamethodisti, Wabatisti, Waprebesteriani, Jeshi la Wokovu. Isa. 55:10-11; Yn. 6:68; Mdo. 13:26; Mdo. 4:12; 1 Kor. 6:11; Gal. 3:26-27; Efe. 5:25-26; Lk. 7:30.

## XVIII. YAHUSUYO SHERIA NA INJILI

**TUNAAMINI** (a) kwamba ili Neno la Mungu lihubiriwe kwa usahihi, ni lazima kuangalia kwa makini tofauti iliyoko kati ya Sheria na Injili; (b) kwamba Sheria hufunua dhambi, hutangaza ghadhabu ya Mungu, huwahukumu wasiomtii Yeye kikamilifu, tena hutoa maagizo kulingana na mapenzi ya Mungu, kuhusu ni nini wanadamu wanapaswa kufanya, na nini hawapaswi kufanya, hata hivyo, pasipo kutoa nguvu ya kufanya matendo mema yanayodaiwa, ili kwamba asiwepo mwanadamu anayeweza kuokolewa kwa matendo ya Sheria; (c) kwamba Injili ni ujumbe wa neema ya wokovu katika Kristo Yesu, ambayo kwayo Roho Mtakatifu huumba imani ndani ya wanadamu na kwa hiyo huwaokoa; (d) kwamba Sheria ihubiriwe katika ukali wake wote na Injili nayo ihubiriwe katika utamu wake wote.

a & b) Rum. 4:15. Kwa sababu Sheria ndiyo ifanyayo hasira; maana pasipokuwa Sheria, hapana kosa.

Gal. 3:21. Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa, kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yakini haki ingalipatikana kwa sheria (Tazama pia Rum. 3:27; Efe. 2:8-9).

Kumb. 27:26. Na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii kuyafanya (Tazama pia Rum. 3:20; Zab. 143:2.
c) 1 Tim. 1:15. Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi.

Yn. 3:16. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Lk. 2:10. Malaika akawaambia, msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote.

d) Gal. 3:10. Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye.

Rum. 1:17. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba Injili pia ni mafundisho yahusuyo matendo mema: Kanisa la Roman Katoliki, Waarmenia, Wamethodisti, Evangelical United Brethren, Evangelical Congregational. 1 Tim. 1:15; Yn. 1:7; Yn. 3:16; (Rum. 10:15; Gal. 1:6-9; Efe. 6:15; 2 Thes. 2:14; 2 Tim. 1:10).

2. Kwamba Injili ni nuru ya ndani ya nafsi inayotolewa kwa wanadamu mara moja ambayo ni kipawa cha Roho Mtakatifu. Quakers,. Lk. 4:18-19; Efe. 1:13; Efe. 2:17; (Rum. 10:17).

3. Kwamba ahadi ya Injili ina masharti, na hutolewa kwa wale wanaomtii Mungu na kuzitii sheria za Kanisa. Kanisa la Roman Katoliki. (Rum. 10:5-8; 11:6); Rum. 4:16; Mdo. 16:31.

4. Kwamba mwanadamu anakuwa Mkristo kwa kuitii sheria: Wamethodisti, Kanisa la Roman Katoliki. Gal. 3:2-5; Gal. 3:21-22; 2 Kor. 3:6.

5. Kwamba hata katika Agano Jipya Wakristo wanapaswa kuzitii (kutawaliwa) na sheria zinazohusiana na sikukuu: Kanisa la Roman Katoliki (sheria za mitume na warithi wao), Kanisa la Orthodox la Mashariki, Wapresbeteriani, Congregational Christians, Free Will Baptists, Wabatisti, Wamenonaiti, Wamethodisti, Evangelical United Brethren, Evangelical Congregational Church, Wamoraviani, Quakers, Wamomeni (sheria za sikukuu kuitakasa Siku ya Sabato zinapaswa kujumuisha siku ya Jumapili), Wasabato (maadhimisho ya Sabato ama Siku ya Saba), Irvingites (sheria zihuzuzo fungu la kumi). Ebr. 10:1; Kol. 2:16; Gal. 5:12-13; Mdo. 15:10, 28-29; Rum. 14:5-6; Gal. 4:10-11; Mk. 2:27; Gal. 5:3; Gal. 2:3-5.

## XIX. YAHUSUYO SAKRAMENTI

**TUNAAMINI** (a) kwamba Sakramenti ni vyombo vya neema vilivyowekwa na Mungu, ambavyo kwa njia ya vitu vionekanavyo vinapounganishwa na Neno lake, Mungu anatoa, kupitisha na kuweka chapa ya neema yake ndani ya wanadamu ambayo Kristo aliwastahilisha kutokana na mateso na kifo chake; (b) kwamba Kristo aliweka Sakramenti mbili tu nazo ni Ubatizo Mtakatifu na Chakula cha Bwana.

a) Yohana 3:5. Yesu akajibu, Amini, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.

Tit. 3:5. Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu.

b) Mat. 28:18-20. Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Mk. 16:15-16. Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.

Lk. 22:19-20. Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula; akisema, kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu (Tazama pia Mat. 26:28).

**TUNAKATAA** mafundisho yafuatayo kwa sababu ni kinyume na Maandiko Matakatifu:

1. Kwamba Kristo aliweka sakramenti zingine tano tofauti na Sakramenti ya Ubatizo na Chakula cha Bwana. Kwamba Sakramenti hizo ni Kipaimara, Kitubio, Upako wa Mwisho, Upadrisho, na Ndoa. Kanisa la Roman Katoliki, Kanisa la Orthodox la Mashariki (Tazama vifungu vya hapo juu).